COLORADO
Department of
Labor and Employment

VIWANGO VYA COLORADO VYA SAA ZA ZIADA NA MALIPO YA CHINI ZAIDI
BANGO LA AMRI ("Amri ya COMPS") #37
Kitengo cha Viwango na Takwimu za Leba

Kuanzia Januari 1, 2021
Ni lazima isasishwe kila mwaka; bango jipya inapatikana wiki ya 1 ya Desemba

Mshahara wa Chini Zaidi Colorado: $12.32 kwa saa, au $9.30 kwa Waajiriwa Wanaopokea Marupurupu, kuanzia 1/1/2021.

- Mshahara wa chini zaidi unabadilika kila mwaka kulingana na mfumuko; Amri na Bango la COMPS la mwaka ujao itaeleza mshahara wa chini zaidi wa 2022.
- Mshahara wa chini zaidi unatumika kwa watu wote wazima na watoto ambao wameshachukua malezi yao wenyewe kisheria, iwe malipo ni kwa saa au kwa msingi mwingine wowote (mshahara, asilimia, kulingana na kazi, n.k) isipokuwa iwe haijajumuishwa na Sheria ya 2 ya Amri ya COMPS. Mtoto ambaye hajachukua malezi yake mwenyewe kisheria anaweza kulipwa 15% chini ya mshahara wa chini zaidi.
- Mshahara wa chini zaidi kitaifa ($7.25) na mishahara yoyote mingine ya chini zaidi katika eneo lako (pamoja na $14.77 jimboni Denver kuanzia 1/1/21) inaweza kutumika.
  Ikiwa kazi inadhibitiwa na sheria kadhaa za mshahara wa chini zaidi na wa muda wa ziada, basi sheria iliyo na mshahar wa juu zaidi au wastani inatumika.

Muda wa ziada: Mara 1½ ya malipo ya kawaida kwa saa zaidi ya 40 kwa wiki, 12 kwa siku au 12 mfululizo.

- Saa katika wiki mbili au zaidi haziwezi kuwekwa katika wastani wakati wa kuhesabu saa za ziada.
- Waajiri wanaweza kukosa muda ambao haukufanya kazi (mara nyingi inatwa "muda wa comp") badala ya malipo ya mara moja na nusu kwa saa za ziada.

Vipindi vya Milo: Dakika 30 bila kudakizwa na bila kazi yoyote, kwa zamu za zaidi ya saa 5.

- NI lazima waajiriwa wasipewe kazi yoyote kamwe, na waruhusiwe kufanya mambo yao ya kibinafsi, ili iwe kwamba vipindi vya milo havitalipwa.
- Ikiwa kazi inafanya vipindi vya milo kuwa vigumu kudakizwa, ni lazima iruhusiwe mwajiriwa ale mlo kazini, na ni lazima alipwe kwa ajili ya muda huo.
- Kwa kiwango kinachowezekana, vipindi vya milo ni lazima viwe angalau saa 1 baada ya kuanza na saa 1 kabla ya kumaliza zamu.

Vipindi vya Mapumziko: Dakika 10, zenye malipo, kila baada ya saa 4.

#Saa za Kazi:	Hadi 2	chini ya 2, hadi 6	chini ya 6, hadi 10	chini ya 10, hadi 14	chini ya 14, hadi 18	chini ya 18, hadi 22	chini ya 22
#Vipindi vya Mapumziko:	0	1	2	3	4	5	6

- Vipindi vya mapumziko si lazima ziwe nje ya mahali pa kazi lakini ni lazima mwajiriwa asifanye kazi wakati huo na ni lazima viwe katikati mwa saa 4 kwa kiwango kinachowezekana.
- Vipindi viwili vya mapumziko vya dakika 5, badala ya kipindi kimoja cha dakika 10, vinaruhusiwa ikiwa waajiriwa na waajiri wamekubaliana kwa hiari na bila kulazimishwa, na ikiwa dakika 5 zinatosha kuenda na kurudi kutoka msalani au mahali kwingine ambapo mapumziko ya kweli yanahitajika.
  Urahisi zaidi wakati wa vipindi vya dakika 5 unapatikana katika kilimo, huduma ya nyumbani ya Medicaid, na kwa pamoja kazi ya makubaliano.
- Waajiri ambao hawaidhinishi na kuruhusu vipindi vya mapumziko ni lazima walipe malipo zaidi kwa muda wa kazi ambao ungetumika katika vipindi vya mapumziko.

Muda Uliofanywa Kazi: Muda ambao waajiriwa wanaruhusu kazi/huduma kutekelezwa kwa manufaa yao ni lazima ulipwe.

- Muda wote kwenye mahali pa kazi, kazini, au katika maeneo teule katika mahali pa kazi (lakini sio tu kuwaruhusu waajiriwa ambao hawako kwenye zamu kusalia kwenye mahali pa kazi), ikijumuisha:
  - kuvaa au kuvua mavazi ya kazi (lakini si mavazi yanayovaliwa nje ya kazi), kusafisha/kujipanga, au kazi nyingine ambapo saa hazihesabiwi;
  - kusubiri majukumu kazini, au kupokea au kushiriki maelezo yanayohusiana na kazi; au
  - ukaguzi wa ulinzi/usalama, kujisajili unapoingia kazini au kuondoka kazini; au
  - kusubiri yoyote ya shughuli zilizo hapa juu.
- Safari kwa ajili ya manufaa kwa mwajiriwa ni saa za kazi; safari za kawaida kati ya nyumbani na kazini si saa za kazi. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu muda wa kusafiri na kulala, tazama Sheria ya 1.9.2.

Mapunguzo, Mikopo, na Ada zinazotozwa Mishahara: Chini ya vikwanzo katika C.R.S. 8-4-105 na chini.

- Rekodi za marupurupu ya hadi $3.02 kwa saa (linayopunguza mishahara ya chini zaidi hadi $9.30) zinaruhusiwa kwa wale ambao mara kwa mara, kwa kawaida wanapokea zaidi ya $30 kwa mwezi kama marupurupu. Ikiwa jumla ya malipo ya saa ukiongeza marupurupu ni chini ya mshahara wa chini zaidi, ni lazima mwajiriwa alipie kiwango kinachokosa.
- Mikopo ya milo inaruhusiwa kwa gharama au thamani (bila kumfaidi mwajiriwa) ya mlo unaokubaliwa kwa hiari.
- Mapunguzo ya malazi yanaruhusiwa ikiwa tu makazi yalikubaliwa na mwajiriwa kwa hiari, haswa kwa manufaa ya mwajiriwa (si mwajiri), yanarekodiwa kwa maandishi, na kuwekewa kikomo cha $25 au $100 kwa wiki (kulingana na aina ya makazi).
- Sare ambazo ni mavazi ya kawaida, bila kitu chochote cha kipekee, si lazima zitolewe; sare zile nyingine ni lazima zitolewe bila gharama yoyote kwa mwajiriwa. Waajiri ni lazima walipie usafishaji wowote maalum, na hawawezi kuagiza dhamana au kufanya mapunguzo kwa ajili ya kuzeeka na kuchakaa kwa kawaida.

Yasiyojumuishwa kwenye Amri ya COMPS: Yote yaliyoorodheshwa katika Sheria ya 2; yale makuu ambayo hayajajumuishwa yameorodheshwa hapa chini.

- Maasifa wakuu/wasimamizi, waajiriwa ambao wanafanya maamuzi ya kiutawala, na wataalamu (Sheria ya 2.2.1-3) wanaolipwa mshahara ambao haujajumuishwa:

2021	2022	2023	2024	Kila Mwaka Baada Ya 2024
$40,500	$45,000	$50,000	$55,000	Mshahara wa mwaka wa awali, mfumuko umezingatiwa

- Wamiliki wa 20%, au katika shirika lisilo la kifaida mwajiriwa aliye na malipo ya juu zaidi na/au cheo cha juu zaidi, ikiwa anahusika moja kwa moja katika menejimenti (2.2.5).
- Waajiriwa wa ufundi wa juu unaohusiana na kompyuta (imebainishwa katika 2.2.10), ikiwa analipwa angalau $28.38 kwa saa.
- Wafanyikazi mbalimbali wanaoishi katika mahali pa kazi, ikijumuisha mamaneja wa mali, wafanyikazi kwenye mashamba makubwa, na wafanyikazi wa nyanjani wa elimu ya kambini/nyanjani (2.2.7).
- Wauzaji mbalimbali, lakini sio wa aina zote (2.2.4, 2.4.1, 2.4.2) na madereva wa teksi (2.2.6).
- Waajiriwa fulani wa usafirishaji wa matibabu na wa hospitalini/makazi ya malezi wana sheria zilizorekebishwa za saa za ziada (2.4.4, 2.4.5).
- Waajiriwa wa ski/snoobodi kuteremka kutoka mlimani, ikijumuisha chakula mlimani lakini sio malazi, hawajumuishwi kwenye saa za ziada za saa 40 (2.4.3).
- Kazi za kilimo (2.3) na baadhi ya kazi za usafirishaji (2.4.6) hazijajumuishwa kwenye saa za ziada na vipindi vya milo, na zina vipindi vya mapumziko rahisi zaidi (kilimo) na hazina (usafirishaji) vipindi vya mapumziko.

Haki za Malalamishi na Kutolipiza Kisasi.

- Kitengo cha Viwango na Takwimu za Leba (maelezo ya mawasiliano yapo sehemu ya chini ya Bango) kinakubali malalamishi na vidokezo kuhusiana na ukiukaji wa COMPS au haki nyingine za mishahara chini ya sheria za kitaifa, jimbo au mitaani. Chaguo nyingine, waajiriwa wanaweza kuandikisha kesi mahakamani.
- Wahusika walio na hatia ya mishahara ambayo haijalipwa wanajumuisha mwajiri kama mhusika, na watu binafsi ambao wanadhibiti operesheni za mhusika.
- Waajiriwa hawawezi kulipiza kisasi kwa kutoa vitisho, kuwalazimisha, au kuwabagua waajiriwa wakiwa na lengo la kusambaratisha, kuhitilafiana, au kuzuia uchunguzi, kesi, malalamishi ya mshahara halisi au unaotarajiwa.
- Ukiukaji sheria za mishahara na kutolipiza kisasi unaweza kuripotiwa kwa Kitengo hiki kama malalamishi au vidokezo bila kujitambulisha.
- Hadhi ya uhamiaji haiathiri haki za mishahara kamwe. Kitengo kitachunguza na kutoa hukumu yake kuhusu malalamishi bila kuuliza, kuripoti, au kuzingatia hadhi. Matumizi ya hadhi ya uhamiaji ili kuhitilafiana na haki ni kinyume cha sheria chini ya Sheria ya Ulindaji Mishahara ya 4.8 na sheria nyingine husika.

Bango hili ni lazima liwekwe mahali ambapo linaonwa kwa urahisi na wafanyikazi, ikijumuisha katika mwongozo wowote uliopo wa mwajiriwa, lishirikiwe na wafanyikazi wanaofanya kazi kupitia mtandao, litolewe kwa lugha nyingine kando na Kiingereza inapohitajika, na libadilishwe kila mwaka.

**Bango hili linatoa muhtasari wa sheria kuu za mishahara katika Amri ya COMPS, lakini sio zote, na haupaswi kutegemewa kama maelezo kamili.
Ili kupata Amri kamili, maelezo ya kina, au maswali, maelezo, au malalamishi kuhusu mishahara na sheria nyingine za leba, wasiliana na:**

Kitengo cha Viwango na Takwimu za Leba, coloradolaborlaw.gov, cdle_labor_standards@state.co.us, 303-318-8441 / 888-390-7936.